

Kukua katika familia yenye afya ni sehemu muhimu ya kukua kwa mtoto wako. Pima uwepo wa sumu ya risasi kwa mtoto wako na nyumba yako ili kuepuka ugonjwa unaosababishwa na sumu ya risasi.

Ni Nini Kibaya Mno Kuhusu Sumu ya Risasi?

Sumu ya risasi inaweza kusababisha:

Matatizo ya Kitabia

Ulemavu wa Kujifunza

Kuharibiwa kwa Uwezo wa Kusikia

Kucheleweshwa kwa Uwezo wa Kusema

Uwezo Mdogo wa Kiakili

Nitajuaje Ikiwa Mtoto Wangu Ana Ugonjwa Unaosababishwa na Sumu ya Risasi?

- Watoto wengi wadogo ambao wana ugonjwa unaosababishwa na sumu ya risasi hawaonekani au kufanya mambo kama walio wagonjwa.
- Njia pekee ya kutambua kwa uhakika ikiwa mtoto wako ana ugonjwa unaosababishwa na sumu ya risasi ni kupima damu yake.
- Zungumza na daktari wa mtoto wako kuhusu kupima damu kwa uwepo wa sumu ya risasi kwa mtoto wako. Maine inahitaji watoto wote kupimwa wanapokuwa na umri wa mwaka 1 na miaka 2.

Ni Nini Husababisha Ugonjwa wa Sumu ya Risasi kwa Watoto?

Vumbi ya sumu ya risasi hutoka kwa rangi ya zamani ya sumu ya risasi inavyoharibika, huharibiwa au kuvurugwa wakati wa matumizi ya kila siku au ukarabati wa nyumbani.



Sumu ya risasi huingia kwenye mikono ya watoto, vitu vya kuchezea na matitibandia ambayo wanaweka vinywani mwao baadaye.



Ni rahisi kwa vumbi kutoka kwa rangi ya sumu ya risasi, vipande vya rangi ya sumu ya risasi na mchanga ulio na sumu ya risasi kuishia kinywani mwa mtoto wako.



Vumbi kutoka kwa rangi ya sumu ya risasi kwenye nyumba za zamani ndio sababu kubwa zaidi inayosababisha ugonjwa unaosababishwa na sumu ya risasi ndani ya Maine.

Mbona Watoto Wadogo Wako kwa Hatari Kubwa Zaidi?

- Vumbi ya sumu ya risasi inaweza kuwa kwenye sakafu, vizingiti vya madirisha na mahali ambapo watoto huweka mikono yao na kucheza.
- Watoto, hasa wale walio na chini ya umri wa miaka 3, mara nyingi huweka mikono yao vinywani mwao na kutambaa kwenye sakafu. Hili linafanya iwe rahisi kwa vumbi ya sumu ya risasi kuingia vinywani mwao.
- Kiasi kidogo mno cha vumbi ya sumu ya risasi kinaweza kumdhuru mtoto mdogo. Watoto wana uwezekano zaidi wa kudhuriwa na sumu ya risasi kwa sababu miili na akili zao zinakua bado.

Linda familia yako. Pima mtoto wako. Pima nyumba yako.

- Angalia tovuti hii: maine.gov/healthyhomes
- Piga simu ili kupata ushauri: 866-292-3474, TTY: Piga simu kwa Maine Relay 711



Hatua Rahisi za Kulinda Mtoto Wako Dhidi ya Sumu ya Risasi

Pata Sumu ya Risasi Iliyo Katika Nyumba Yako

- Ikiwa unaishi katika nyumba iliyojengwa kabla ya 1950, agiza kifaa cha bila malipo cha kupima uwepo wa sumu ya risasi kutoka kwa maine.gov/healthyhomes. Hili litakusaidia kugundua ikiwa una vumbi ya sumu ya risasi kwenye nyumba yako.
- Kagua madirisha ambayo yamepakwa rangi, milango, na ikiwa sakafu zimeambuka, zina vipande vidogo vya rangi au rangi inayobambuka. Weka watoto mbali na sehemu zozote ambazo zina rangi iliyoharibika. Tumia fanicha kuzuia maeneo.
- Mwambie meneja wa jengo lako au mmiliki kuhusu rangi ambayo imeharibika ili iweze kukarabatiwa kwa usalama.
- Jifunze jinsi ya kudhibiti vumbi ya sumu ya risasi kabla ya kuanza ukarabati wowote wa nyumba au mradi wa kupaka rangi.
- Ajiri “kontrakta wa RRP ambaye amethibitishwa na EPA” kufanya kazi hiyo. Jifunze zaidi kwenye epa.gov/lead.

Osha Vumbi ya Sumu ya Risasi

- Safisha sakafu, vizingiti vya madirisha na sehemu za juu za meza mara moja kwa wiki kwa fagio zilizo na maji au vitambaa vinavyotupwa baada ya matumizi.
- Fagio, vitambaa vikavu, na vifaa vya kuvuta vumbi visivyo na vichujio vya HEPA hueneza vumbi ya sumu ya risasi.
- Osha mikono ya mtoto wako kwa sabuni na maji kabla ya kula na kulala. Osha vitu vya kuchezea mara moja kwa wiki na kuhakikisha vitu vya kuchezea haviko karibu na maeneo yaliyo na rangi ambayo imebambuka.
- Osha matitibandia na chupa ikiwa zitaanguka kwenye sakafu kabla ya kumpatia mtoto wako.

Usilete Sumu ya Risasi Nyumbani Kwako

- Ikiwa huwa unatumia sumu ya risasi kwenye kazi yako, badilisha viatu vyako na mavazi yako mara moja. Fua nguo za kazi kando na nguo za familia. Oga kabla ya kumgusa mtoto wako.
- Tumia mkeka wa mlango ili kuzuia vumbi kuingia kwenye nyumba yako na kuacha viatu mlangoni.
- Hakikisha kwamba vitu vya sanaa za kale au vitu vya zamani vya kuchezea ambavyo vimepakwa rangi viko katika hali nzuri na kuviweka mahali ambapo haviwezi kufikiwa na watoto. Epuka kutumia dawa za mitishamba ambazo zinaweza kuwa na sumu ya risasi.

Linda familia yako. Pima mtoto wako. Pima nyumba yako.

- Angalia tovuti hii: maine.gov/healthyhomes
- Piga simu ili kupata ushauri: 866-292-3474, TTY: Piga simu kwa Maine Relay 711

